# Hongera TRA kutoa EFD bure, lakini...




Wafanyabiashara katika eneo la Maili Moja Kibaha mkoani Pwani wakijadiliana baada ya kufunga maduka kupinga matumizi ya mashine za kieletroniki (EFD) za kutolea stakabadhi. **Picha ya Maktaba**

Alawi Masare ,Mwananchi

Kwa muda mrefu kuna mgogoro unafukuta kati ya Serikali na wafanya biashara kuhusu matumizi ya mashine za kielektroniki za kukusanyia Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mojawapo ya mambo yaliyokuwa yakisababisha sintofahamu kati ya TRA na wafanyabiashara nchini ni gharama za ununuzi wa mashine hizo za EFD.

Wafanyabiashara walitakiwa kununua mashine hizo zinazouzwa kati ya Sh600,000 na Sh1.2 milioni kwa gharama zao kisha kurejeshewa fedha zao na TRA kupitia kodi inazokusanya.

Hata hivyo, wafanyabiashara kupitia jumuiya zao wamekuwa wakiitaka TRA kuwapatia mashine hizo bure ili kurahisisha kazi badala ya kuwatwisha mzigo usiowahusu wa kuzinunua.

Mgogoro huo ulisababisha hata kufungwa kwa maduka mara kadhaa nchini, hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma kwa wananchi, hasara kwa wafanyabiashara na kukwamisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Hivi karibuni, Rais John Magufuli alikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara nchini na kueleza wazi kwamba ilikuwa imani yake kuwa mashine hizo zingetolewa bure kwa wafanyabiashara.

Baada ya kauli hiyo, TRA nayo ikatangaza takriban wiki mbili zilizopita kuwa mashine hizo ziitatolewa bure kwa wafanyabiashara nchini.

Tangazo hili linaonekana kama mafanikio kwa sekta binafsi na wafanya biashara kutokana na moja ya matakwa yao ya muda mrefu kusikilizwa na Serikali.

### SAUTI ZA WANANCHI

**Salum Mtolela:**

**Mfumo wa kodi wa Tanznia unamdidimiza mfanyabiashara. Utakuta mfanyabiashara ananunua gari China au Japan, kodi ya bandarini inakuwa sawa na bei ya kununulia gari, au ananunua vitu Zanzibar kodi ya bandarini inapita mzigo kumbe wanakukomoa ili utoe rushwa. Cha msingi, Serikali yetu ijenge mazingira mazuri ya kukusanya kodi bila kujenga mazingira ya rushwa.**

**Pius Makundi:**

**Duniani kote hakuna nchi ambayo Serikali yake ilifanya kila kitu yenyewe kama kujenga viwanda na miradi mingineyo, pasipokuwa na sera ya kuwashirikisha wafanyibiashara wa ndani na nje.**

**Ili nchi ipige hatua za mafanikio ya kiuchumi, kwanza inafaa kutengeneza mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa kuwa vyanzo imara vya nishati (umeme) wa uhakika, miundo mbinu kama barabara.**

**Vilevile kuwa na sheria madhubuti za kupambana na rushwa zinazoombwa na watumishi wa umma wasio waaminifu na kupunguza gharama za kodi kwa mfanyabiashara. Imani yangu haya yakisimamiwa kikamilifu, Tanzania itakuwa sehemu salama kwa mfanyabiashara kuweke-**

**Changamoto za EFD**

Hata hivyo, bado kuna changamoto lukuki ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili matumizi ya mashine hizo yawe thabiti.




Mashine za kieletroniki za kukusanyia kodi (EFD) kwa wafanyabiashara nchini. **Picha ya Maktaba**

Utafiti uliofanywa na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Morogoro mwaka 2012, ulibaini changamoto kadhaa ambazo hadi sasa hazijatatuliwa.

Utafiti huo ambao ulifadhiliwa na Taasisi ya Kutetea Mazingira Bora ya Ufanyaji Biashara (BEST-AC) ulifanyika katika mikoa ya Morogoro, Njombe, Iringa na Dar es Salaam.

Baadhi ya mambo yaliyoibuka katika utafiti huo ni pamoja na miundombinu dhaifu hasa ile ya umeme, hali inayosababisha kukatika kwa nishati hiyo mara kwa mara na hivyo EFD kushindwa kufanya kazi; ugumu katika kuunganisha mifumo ya TRA na ile ya kihasibu ya kampuni za biashara; na kukosekana kwa mawasiliano katika baadhi ya maeneo na ikizingatiwa kwamba mashine hizo hutumia mitandao ya simu.

Changamoto nyingine ni uduni wa mashine zenyewe zinazotoka nje ya nchi na kukosekana makubaliano kuhusu matengenezo yake, hivyo kusababisha usumbufu na gharama za kucheleweshwa matengenezo.

Utafiti huo ulibaini kwamba katika mzunguko wa biashara wa mwaka mmoja, mfanyabiashara hutumia siku 54 kushughulikia matengenezo ya mashine na changamoto nyingine za kiufundi ambazo huzipata EFDs.

"Kutokana na msongamano na kushindwa kutuma taarifa kwa wakati, mfanyabiashara atapoteza kwa wastani siku nyingine 22 ndani ya mwaka huohuo. Gharama za kupiga simu kwenda TRA na wasambazaji wa mashine hizi zinafika kati ya Sh54,000 na Sh108,000 kwa mwaka," ilisema ripoti ya utafiti huo na kuongeza:

"Sekta binafsi haikatai kulipa kodi. Inachokitaka ni kuwapo mfumo wa ulipaji kodi ulio wazi, rahisi, wa haki na usiyo mzigo kwa wafanya biashara ambao tunaamini utaongeza ufanisi na kupunguza usumbufu katika ukusanyaji kodi."

Ilikadiriwa kwamba kama biashara zote zingeunganishwa na EFD zingetumika kwa ufanisi wake, TRA ingeweza kuongeza mapato ya Serikali kwa karibu asilimia 50.

Utafiti huo pia ulibaini changamoto nyingine ya wafanyabiashara wengi kutojua hata sheria na kanuni zinazosimamia EFD na badala yake wamekuwa wakiongozwa na maelekezo ya maofisa wa TRA na wasambazaji wa mashine hizo.

Changamoto nyingine iliyobainishwa ni kwamba wafanya biashara wengi hawakujengewa uwezo wa kutosha juu ya matumizi ya EFD, hali iliyowafanya kukosea mara kwa mara ikiwamo kuingiza miamala isiyo sahihi na hivyo kuwasababishia hasara.

Kuhusu ubora hafifu wa EFD, utafiti ulisema asilimia 59.3 ya watumiaji wa mashine hizo walitoa taarifa za kuwapo matatizo ya ufanyaji kazi.

Licha ya kuwapo changamoto ya kukatika umeme mara kwa mara, mashine hizo zimeripotiwa kuwa na betri ambazo hazikai na umeme (chaji) kwa muda mrefu ili kuwawezesha wafanyabiashara kuzitumia hata wakati umeme umekatika.

Kwa mujibu wa utafiti huo, EFD hutumia laini za simu na katika baadhi ya maeneo mtandao huwa na shida, hivyo kuathiri shughuli za wafanyabiashara.

**Kwa maoni kuhusu mazingira ya kibiashara Tanzania tuma ujumbe 0786240172. Ujumbe utakaochapishwa utazawadiwa Sh30,000 za muda wa maongezi.**

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA

BEST-Dialogue

Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo